National Investments PLC
50 Mirambo Street
3rd Floor, Mirambo House
P.O. Box 7465
Dar Es Salaam
Phone: +255 22 2111399/ +255 733 006 177
WhatsApp 0733 006 177
E-mail: invest@nicol.co.tz

*The Economic Shield of the Nation*

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MOJA (11) WA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja (11) wa mwaka wa Wanahisa wa National Investments PLC (NICOL) utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 30 Agosti 2025 kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mkutano utafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali. Dawati la usajili wa wanahisa litafunguliwa mapema kuanzia saa mbili (2:00) asubuhi.

**Ajenda ya Mkutano ni Kama Ifuatavyo:**

11.1. MATANGAZO NA AKIDI YA MKUTANO.

11.2. KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO MKUU WA KUMI (11).

11.3. KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI (10) ULIOFANYIKA TAREHE 28 SEPTEMBA 2024.

11.4. YATOKANAYO NA MKUTANO WA KUMI (10) WA WANAHISA.

11.5. KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024.

11.6. KUIDHINISHA GAWIO LA MWAKA WA FEDHA 2024.

11.7. KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI.

11.8. KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI

11.9. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2025.

11.10. MENGINEYO.

**MAELEZO MUHIMU:**

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano ni lazima wawasilishe nakala ya kitambulisho kama kitambulisho cha Taifa, kitambulisho cha mpiga kura, hati ya kusafiri au leseni ya Udereva.
2. Tarehe ya kufunga Daftari la Wanahisa wanaostahili kushiriki mkutano itakuwa Ijumaa tarehe 22 Agosti 2025.
3. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria mkutano na kupiga kura ana haki ya kuteua mwakilishi ahudhurie kwa niaba yake, iwapo yeye atashindwa kufanya hivyo, kwa kuzingatia vipengele vya kanuni za kampuni.
4. Nakala za Taarifa ya Mwaka na fomu za uwakilishi zitapatikana katika ofisi ya NICOL au kwa kutembelea tovuti ya NICOL **www.nicol.co.tz.** Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi za NICOL zilizopo Ghorofa ya 3, Mirambo House, Mtaa wa 50 Mirambo Dar es Salaam au kwa barua pepe **invest@nicol.co.tz** kabla ya saa 10 jioni, siku ya Alhamisi tarehe 28 Agosti 2025.
5. Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia namba zifuatazo: 0733 006 177, 0768 00 88 00 au +255 22 2111 399 na WhatsApp 0768 00 88 00 au 0733 006 177.

**Kwa idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.**

______________________________

**Adv. Benjamin Mwakagamba**
Katibu wa Kampuni
**NATIONAL INVESTMENTS PLC**
**24 Julai 2025**